AZIMIO NA. 4/2014

AZIMIO LA BUNGE LA KURIDHIA ITIFAKI YA KUANZISHWA KWA TUME YA UTAFITI WA AFYA YA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI

KWA KUWA, Nchi za Kenya, Tanzania na Uganda zina historia ya ushirikiano katika Nyanja za biashara, viwanda na utamaduni;

NA KWA KUWA, Mwaka 1967 – 1977 nchi hizi ziliunda Jumuiya ya Afrika Mashariki ambapo nchi Wanachama ziliweza kunufaika na huduma mbalimbali zilizokuwa zikitolewa chini ya Jumuiya hiyo;

NA KWA KUWA, Huduma mojawapo ilikuwa ni ya Baraza la Utafiti wa Tiba la Afrika ya Mashariki *(East African Medical Research Council)* ambalo lilianzishwa mwaka 1963, ili kuratibu na kusimamia tafiti za afya katika nchi wanachama;

NA KWA KUWA, Tanzania (wakati huo ikiitwa Tanganyika) ilikuwa na Taasisi ya Utafiti wa Tiba ya Afrika Mashariki (Mwanza) na Taasisi ya Malaria na Vidudu enezi vya magonjwa (Amani) na kwa upande wa Kenya kulikuwa na Kituo cha Utafiti wa Kifua Kikuu Afrika Mashariki (Nairobi) na Kituo cha Maabara ya Utafiti wa magonjwa ya Binadamu; na Uganda kulikuwa na

Taasisi ya Utafiti wa Virusi (Entebbe) na Kituo cha Utafiti wa Malale (Tororo);

NA KWA KUWA, Mabaraza na Taasisi zote zilizoundwa katika Nchi Wanachama, zilikuwa chini ya Mfumo wa Shirika la Kikanda la Utafiti wa Afya;

NA KWA KUWA, kutokana na kuvunjika kwa Jumuiya hiyo mwaka 1977, mfumo huo wa Shirika la Kikanda la Utafiti wa Afya ambalo lilijumuisha Baraza la Utafiti wa Tiba la Afrika Mashariki nalo lilivunjika na kila nchi iliunda taasisi yake;

NA KWA KUWA, Tanzania iliunda Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) mwaka 1979 kwa Sheria ya Bunge Na. 23;

NA KWA KUWA, Mwaka 1999 Kenya, Tanzania na Uganda ziliwekeana mkataba wa kuanzisha tena Jumuiya ya Afrika Mashariki baada ya kuwa zilifaidika na huduma zilizokuwa zinatolewa chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya awali kati ya mwaka 1967 hadi 1977;

NA KWA KUWA, baada ya kuundwa upya kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1999, Nchi Wanachama ziliamua kufufua ushirikiano katika maeneo ya afya, huduma za jamii na utamaduni, hususan katika utafiti wa afya na sera ya afya;

NA KWA KUWA, Baraza la Mawaziri la Nchi Wanachama liliunda Baraza la Kisekta katika masuala ya afya na Baraza hilo lilikubaliana kuanzisha

chombo cha kuratibu na kuainisha Agenda za Kikanda za ushirikiano katika utafiti wa afya na ubadilishanaji wa matokeo ya tafiti pamoja na kupeana taarifa za tafiti mbalimbali;

NA KWA KUWA, Nchi Wanachama zilidhamiria kushughulikia masuala ya tafiti za afya na matokeo yake kwa ajili ya teknolojia na utoaji wa huduma za afya endelevu na kutafsiri matokeo ya tafiti za afya katika maandalizi ya sera na utoaji wa huduma za afya;

NA KWA KUWA, Tanzania imeonyesha nia yake ya kuendelea na huduma hii baada ya kuanzishwa upya kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kuweka saini Itifaki ya Kuanzishwa Tume ya Utafiti wa Afya Afrika Mashariki tarehe 13 Septemba, 2008;

NA KWA KUWA, Ibara ya 29 ya Itifaki hii inazitaka nchi zote wanachama kuridhia na kuwasilisha mapendekezo na Hati ya Kuridhia kwa Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki;

NA KWA KUWA, hadi sasa nchi ya Uganda na Kenya, tayari zimeridhia Itifaki hii na Burundi na Rwanda kuikubali, Tanzania ni nchi pekee ambayo bado haijaridhia Itifaki ya kuundwa kwa Tume hii;

NA KWA KUWA, Tanzania kwa kuweka saini Itifaki hii na hatimaye kuitekeleza itanufaika na mambo yafuatayo:-

(a) Kuboresha uhusiano na uratibu katika shughuli za utafiti wa afya na kutoa miongozo ya pamoja itakayotumiwa na nchi wanachama katika kuandaa rasimu na utoaji vibali vya utafiti;

(b) Kuhamasisha tafiti za pamoja na baina ya nchi wanachama ili kuweza kupata njia za pamoja kukabiliana na magonjwa yanayokabili nchi wanachama;

(c) Kuhamasisha na kuharakisha matumizi ya ushahidi wa kisayansi na kitafiti ili kuboresha utungaji na utekelezaji wa sera katika sekta ya afya;

(d) Kuwa na misingi na uratibu wa uendelezaji wa rasilimali watu katika tatifi za kiafya;

(e) Kuendeleza ubadilishanaji wa taarifa za tafiti za afya baina ya nchi wanachama;

(f) Kufanya ukaguzi wa miradi mbalimbali ya kitafiti ya afya ndani ya nchi wanachama;

(g) Kuwa na kiungo cha wahisani wa maendeleo katika masuala ya tafiti za afya, waliopo ndani ya nchi wanachama, kikanda na kimataifa;

(h) Kuwa na utaratibu wa pamoja wa kushughulikia masuala ya haki na hati miliki zinazohusiana na masuala ya utafiti wa afya;

(i) Watalam kunufaika na nafasi za ajira zitakazopatikana katika Makao Makuu ya Tume na kuweza kuibua fursa na kufanya tafiti za afya zilizo bora;

(j) Kuanzishwa rasmi kwa Tume ambayo Makao Makuu yake yatakuwa Burundi kama ilivyoamuliwa na Kikao cha Mawaziri wa Afya wa Nchi Wanachama kilichofanyika Bujumbura tarehe 21 hadi 26 Novemba, 2011;

HIVYO BASI, kwa kuzingatia umuhimu na manufaa ya Itifaki hii kwa Tanzania, Bunge hili katika Mkutano wa Kumi na Sita na Kumi na Saba na kwa mujibu wa Ibara ya 63 (3) (e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania ya Mwaka 1977, linaazimia kuridhia Itifaki ya Kuanzisha Tume ya Utafiti wa Afya ya Afrika Mashariki yaani *the Protocol on the Establishment of the East African Research Commission*.

Limepitishwa na Bunge leo tarehe 14 Novemba, 2014.

Dkt. T. D. Kashililah
KATIBU WA BUNGE